


ASb
approved



Punda na Fahali

Ursula Nafula


Salim Kasamba

Kiswahili






Mukulima alikuwa na Fahali mzee.




Pia, alikuwa na Punda.

Fahali na Punda walikuwa marafiki.




Mwisho wa siku, Fahali alimwambia Punda, "Leo nimechoka sana."




Siku iliyofuata, Fahali tena alilalamika, "Leo sikupumzika hata kidogo."



Punda alimjibu, "Nilienda sokoni. Kazi yangu ilikuwa ngumu kuliko yako."



Kesho yake Fahali alisema tena, "Leo ilikuwa siku mbaya kwangu."



Punda alimjibu, "Mkulima akija, mlilie, 'Moo! Moo!'
Atakuruhusu upumzike."




Fahali alimlilia mkulima, "Moo! Moo!"

Mkulima alimruhusu akapumzika.




Mkulima alimfunga Punda jembe.

Punda alilima badala ya Fahali.




Punda alifanya kazi siku nzima.

Jioni, alikuwa amechoka sana.



Punda alisema, "Mkulima ameamua kukuchinja. Unachoka sana tena u mgonjwa."



Fahali alimjibu Punda, "Kesho nitafanya kazi yangu.
Nimepata nafuu."

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way: Melese Getahun Wolde and Elizabeth Laird

Author - Melese Getahun Wolde and Elizabeth Laird

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Salim Kasamba

Language - Kiswahili

Level - First words © African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com

